# SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 24 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) FEBRUARI 2023

# SILINDE AITAKA TSC KUTUMIA VIZURI FEDHA ZA MRADI WA BOOST




*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (wa tatu kutoka kulia) akikata utepe kuashiria uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Januari 24, 2023 mjini Morogoro.*

**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania

# ASANTE RAIS SAMIA KWA KUENDELEA KUFANYA MAPINDUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU

Ni ukweli usiopingika kuwa moja kati ya mafanikio tunayoyaona nchini ni matunda ya juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutafuta wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Kati ya mafanikio ya miradi ya maendeleo ni pamoja na mradi wa BOOST unafadhiliwa na Benki ya Dunia.

BOOST ni sehemu ya Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu ya awali (EPforR II) na inachangia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

Kupitia Mradi huu, Rais wetu ameridhia kiasi cha Shillingi Trilioni 1.15 zielekezwe kwenye Sekta ya Elimu katika kuboresha zaidi Elimu ya Msingi.

Fedha hizo zitatumika kujenga madarasa 12,000, kuhakikisha shule 6,000 zinakuwa na Mpango wa Shule Salama, kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali kutoka asilimia 75 hadi kufikia asilimia 85, kuimarisha Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA), kununua vifaa vya TEHAMA kwa Shule zaidi ya 800 za Msingi na Vituo vya Walimu kwa ajili ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji na mafunzo endelevu ya Walimu kazini. Mradi huu utatekelezwa kwa awamu kwa muda wa miaka mitano (5) kuanzia 2021/2022 hadi 2025/26.

Kila mmoja wetu ana kila sababu ya kumshukuru na kumpongeza Rais wetu kwa jitihada zake za kuboresha elimu nchini. Pia tunawashukuru Wadau wetu wa Maendeleo kwa namna wanavyoendelea kuziunga mkono juhudi za Serikali yetu kuwaletea maendeleo wananchi.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma Muya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI



# SILINDE AITAKA TSC KUTUMIA VIZURI FEDHA ZA MRADI WA BOOST



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (wa kwanza kushoto) akimkabidhi Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu hicho uliofanyika Januari 24, 2023 mjini Morogoro. Katikati kwa Mwenyekiti na Katibu wa TSC ni Naibu Waziri wa OR - TAMISEMI, Mhe. David Silinde.*

**Na Mwandishi Wetu - Morogoro.**

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde ameitaka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuhakikisha inatumia vizuri fedha za Miradi wa BOOST ili ziweze kuleta tija katika maendeleo ya utumishi wa walimu nchini.

Silinde ameyasema hayo Januari 24, 2023 mjini Morogroro kwa niaba ya Waziri wa Nchi OR – TAMISEMI wakati akizindua Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kilichoandaliwa na TSC kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa BOOST ambapo uzinduzi huo umeambatana na Kikao kazi cha siku nne kinachowakutanisha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya zote Tanzania Bara.

“Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, amesisitiza sana fedha hizi za Mradi zitumike kwa Uadilifu na Uzalendo wa hali ya juu ili kuleta tija na kuwa na matokeo chanya ambayo yatawezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo. Niwaombe sana wote tushirikiane vyema katika utekelezaji wa Mradi huu ili kuleta ufanisi uliokusudiwa katika sekta ya elimu. Niwasihi kutokubadilisha matumizi ya fedha za Mradi kinyume cha shughuli zilizopangwa,” amesema Naibu Waziri Silinde.

Akizungumzia kuhusu Kitabu hicho, Naibu Waziri Silinde amesema kuwa, kutokana na kuwepo kwa mabadiliko ya Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu,



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde akizungumza na Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC (hawapo pichani) wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Januari 24, 2023 mjini Morogoro.*

# SILINDE AITAKA TSC KUTUMIA VIZURI FEDHA ZA MRADI WA BOOST



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (hayupo pichani) wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Januari 24, 2023 mjini Morogoro.*

Utandawazi na ongezeko la idadi ya Walimu ni wakati sahihi kwa TSC kufanya mapitio na kutoa ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendeji Kazi katika Utumishi wa Walimu unaoendana na mabadiliko hayo.

Ameongeza kuwa ili kutimiza malengo ya kuwa na Shule Salama ni lazima kuhakikisha kuwa kila mwalimu anatambua na kutekeleza wajibu wake kwa kuzingatia Maadili ya kazi yake ikiwa ni pamoja na kumlea mwanafunzi kimwili, kiroho, kiakili, kisaikolojia na kijamii pamoja na kuwajibika katika taaluma yake, kwa mwajiri, jamii na Taifa kwa ujumla.




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu Januari 24, 2023 mjini Morogoro.*

Kutokana umuhimu wa uzingatiaji wa Maadili, Naibu Waziri huyo ameiagiza TSC kuhakikisha Walimu wote nchini wanajengewa uwezo kuhusu Kanuni za Maadili ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa kuzingatia ufafanuzi huo pamoja na kuandaa utaratibu wa kuwaelimisha walimu wapya wanapoajiriwa ili wanaposaini Mikataba ya Ajira wasaini pia kukubali kutekeleza Kanuni hizo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba amesema kuwa ni muhimu kuhakikisha walimu wanasaidiwa kufahamu maadili ya kazi yao ili waweze kuandaa wanafunzi wenye weledi katika taaluma zao pamoja na kuwa na maadili mema katika jamii huku akisisitiza kuwa mwanafunzi asiyekuwa na maadili hata akifanya vizuri kitaaluma bado ni hasara kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Tunaahidi kuwa Tume itaendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia Utumishi na Maadili ya Walimu kwa lengo la

# SILINDE AITAKA TSC KUTUMIA VIZURI FEDHA ZA MRADI WA BOOST

kuhakikisha kuwa tunakuwa na Walimu wanaozingatia Maadili kwa ajili ya kuwalea Watoto wetu na hatimaye kuboresha elimu nchini," alisema Prof. Komba.

Naye Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama amesema Tume ya Utumishi wa Walimu ni miongoni mwa Taasisi zinazotekeleza Mradi wa BOOST ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia na kupitia Mpango wa Shule Salama, Tume hiyo imewezeshwa kufanya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa mujibu wa Kifungu cha 5 (j) cha Sheria Sura Na. 448.

Ameongeza kuwa kupitia mradi wa BOOST TSC imewezeshwa pia kufanya Mapitio ya Sheria na Kanuni zinazomhusu Mwalimu, Kununua vitendea kazi vikiwemo Kompyuta na Magari na kuwajengea uwezo Watumishi wa Tume hiyo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao.

"Tume ina jukumu la msingi la kusimamia Maadili ya Kazi ya Ualimu chini ya Kifungu cha 5(c) cha Sheria Sura ya 448. Kifungu cha 5(j) cha Sheria hiyo kimeipa Tume jukumu la kutoa ufafanuzi kuhusu Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu. Hivyo, kutokana na matakwa ya Kanuni hizo na uwepo wa mabadiliko ya kisera, Sheria, Kanuni na Utandawazi, Tume iliona umuhimu wa kurejea Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu na kuzitolea ufafanuzi," amesema.

Ameongeza kuwa ufafanuzi kuhusu Kanuni hizo umeandaliwa na kuidhinishwa na Tume baada ya kupitia michakato mbalimbali ikiwemo ushiriki wa wadau kutoa maoni yao, uhariri wa nyaraka husika huku akieleza kuwa kazi ya kutafsiri ufafanuzi huo kwa lugha ya Kiingereza inaendelea.

Kwa mujibu wa Mwl. Nkwama, uzinduzi wa kitabu hicho ni hatua ya msingi ya kuhakikisha kuwa walimu wanazingatia maadili ya taaluma yao katika kutekeleza majukumu yao ili kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na Mpango wa Shule Salama.

"Tume ina matarajio makubwa kwamba baada ya uwepo wa Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi wa Utumishi wa Walimu, changamoto mbalimbali za ukiukwaji wa Maadili ya Kazi ya Ualimu kwa walimu zitapungua au kuisha kabisa na hivyo kuifanya kazi ya Ualimu iendelee kuwa na hadhi yake inavyotakiwa" amesema Nkwama.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia elimu katika Mkoa huo, Mwl. Germana Mung'aho amesema kuwa Ufafanuzi huo ukizingatiwa vizuri walimu wote watakuwa na maadili mema na hivyo itaondoa dhana iliyojengeka kuwa walimu wa zamani ndio wenye maadili zaidi kuliko walimu wanaoajiriwa sasa.



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde akikabidhi Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa mmoja wa Kaimu Katibu Wasaidizi mara baada ya uzinduzi wa Kitabu hicho uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro.*

# SILINDE AITAKA TSC KUTUMIA VIZURI FEDHA ZA MRADI WA BOOST



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde akikabidhi Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwa mmoja wa Kaimu Katibu Wasaidizi mara baada ya uzinduzi wa Kitabu hicho uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro.*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (kulia) akimkabidhi Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu mara baada ya uzinduzi wa Kitabu hicho uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro.*









*Washiriki wa kikao kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC wakiwa katika kikao hicho kinachofanyika Januri 24 – 27, 2023 mjini Morogoro.*

# Bi. Fatuma Muya

## Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu

**Jarida la Sauti ya TSC linakupongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nafasi ya Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu (DTAED) Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).**

"Tunakuombea utekeleze majukumu yako mapya kwa bidii, ufanisi weledi na Uzando ili walimu waendelee kupata huduma bora."

**Kazi iendelee.**



# TSC YAANZA KUTEKELEZA MPANGO WA SHULE SALAMA KWA KUFANYA MAPITIO YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI YA WALIMU



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akifungua kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kupitia Rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.*

**Na Mwandishi Wetu - Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa walimu (TSC) imefanya kikao na wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo la kupitia na kufanya maboresho ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Akizungumza katika kikao kazi hicho kilichowakutanisha wadau wa elimu kwa siku nne kuanzia Januari 10 - 13, 2023 mjini Morogoro, Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba amesema TSC inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona suala la maadili ya walimu linahitaji kupewa kipaumbele na kuamua sehemu ya fedha za mradi wa BOOST zielekezwe kwenye eneo hilo.

"Tume ya Utumishi wa Walimu pamoja na wadau mbalimbali wa elimu tunamshukuru sana Rais wetu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona maadili ya walimu ni moja ya mambo yanayopaswa kupewa kipaumbele katika mradi huu wa BOOST. Maadili ya walimu ni muhimu kwa kuwa mwalimu ndiye anayemtengeneza mwanafunzi kuwa raia mwema au raia asiyefaa katika jamii," alisema Prof. Komba.

Aliongeza kuwa kutokana




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la utangulizi katika kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kujadili rasimu ya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.*

# TSC YAANZA KUTEKELEZA MPANGO WA SHULE SALAMA KWA KUFANYA MAPITIO YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI YA WALIMU




*Mmoja wa Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Jane Mtindya akitoa neno la kumkaribisha mwenyekiti wa Tume (hayupo pichani) kwa ajili ya kufungua kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kupitia Rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.*

maana. Mwanafunzi anaweza kupata Daraja la kwanza lakini akiingia mtaani anakuwa mwizi, mla rushwa, mtu asiye na heshina, mtumia madawa ya kulevya, nk, hapo taaluma yake haina maana kwa kuwa anakuwa ni hasara kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Hivyo, suala la maadili ni jambo muhimu sana katika taaluma ya Ualimu," alisema Prof. Komba.

Prof. Komba pia aliongeza kuwa suala la kufanya ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ni muhimu litasaidia kuelezea kanuni hizo katika lugha rahisi ambayo itafanya walimu kuielewa na kuzingatia maadili hayo katika utendaji kazi wao, hivyo aliielekeza Menejimenti ya Tume hiyo kuhakikisha kazi hiyo na umuhimu ambao Rais aliuonesha katika eneo hilo, TSC ina jukumu kubwa kuhakikisha inasimamia walimu kwa karibu na kuwakumbusha mara kwa mara kuzingatia taratibu na miiko ya taaluma hiyo katika kuwalea wanafunzi.

Prof. Komba aliendelea kueleza kuwa kwa kiasi kikubwa walimu wamejikita zaidi katika kufundisha wanafunzi masomo ya darasani na kuhakikisha wanafaulu katika mitihani yao huku wakisahau kujenga wanafunzi katika maadili mema yanayowaandaa kuwa raia wema katika jamii na Taifa kwa ujumla.

"Mwanafunzi asiyekuwa na Maadili hata akifaulu vizuri haina



*Washiriki wa kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kujadili rasimu ya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu wakiwa wanaendelea na kikao.*

# TSC YAANZA KUTEKELEZA MPANGO WA SHULE SALAMA KWA KUFANYA MAPITIO YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI YA WALIMU



*Washiriki wa kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kujadili rasimu ya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu wakiwa wanaendelea na kikao.*

"Tume ya Utumishi wa Walimu chini ya Ofisi ya Rais- TAMISEMI ni watekelezaji wa shughuli za Mradi wa BOOST ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia ambapo katika utekelezaji wa shughuli za Mradi huo, Tume imewezeshwa, kununua vitendea kazi vikiwemo Kompyuta na Magari pamoja na kujengea uwezo watumishi wa TSC kuhusu utekelezaji wa majukumu yao."

"Napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuwa na Miradi ya Maendeleo ambapo leo Tume kupitia Mradi wa BOOST imeweza kufanikisha kwa sehemu kubwa utekelezaji wa majukumu yake."

inafanyika kwa weledi na ufanisi ili kufikia malengo yaliyotarajiwa.

Pamoja na hayo, Mwenyekiti huyo aliiagiza Sekretarieti ya Tume hiyo kuhakikisha inatoa elimu kwa walimu na wadau wengine kuhusu ufafanuzi wa Kanuni hizo ili kuwasaidia walimu kujiepusha na ukiukwaji wa maadili ya kazi yao kitu ambacho kinasababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa kazi.

Akitoa neno la utangulizi, Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama amesema Tume imewezeshwa kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Miiko ya kazi ya Ualimu ili kutoa ufafanuzi wa kanuni hizo ziweze kueleweka kirahisi na watumiaji ambao ni walimu.



*Washiriki wa kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kujadili rasimu ya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu wakiwa wanaendelea na kikao.*

# TSC YAANZA KUTEKELEZA MPANGO WA SHULE SALAMA KWA KUFANYA MAPITIO YA UFAFANUZI WA KANUNI ZA MAADILI YA WALIMU

"Ninapenda kumpongeza pia Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Katibu Mkuu kwa kuona umuhimu wa Tume kuwezeshwa na Mradi huo ili kutekeleza majukumu yake ambayo moja kwa moja yanamlenga Mwalimu kwa ajili ya kuleta matokeo chanya kwa mwanafunzi shuleni, pia ninawashukuru Benki ya Dunia ambao wanasimamia utekelezaji wa Mradi kwa kuridhia Tume kuwa watekelezaji wa shughuli za Mradi," alisema Nkwama.

Alieleza kuwa Mradi wa BOOST utekelezaji wake umejikita katika Afua nane ikiwemo Afua ya Mpango wa Shule Salama na kueleza kuwa Mwalimu anayezingatia Maadili na Miiko ya kazi yake ana mchango mkubwa katika kuifanya Shule iwe salama, hivyo, kupitia Mradi huo, Tume imezeshwa kufanya mapitio ya Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu na kuandaa rasimu ambayo imewasilishwa katika kikao kazi hicho kwa ajili ya kupata maoni ya wadau.

Kwa mujibu wa Nkwama, kumekuwa na ongezeko la baadhi ya walimu wanaojihusisha na vitendo vya ukiukaji wa maadili ya kazi ya ualimu na hivyo kufanya kazi ya ualimu ipoteze hadhi yake, hivyo TSC ambayo ni mamlaka katika kumsimamia Mwalimu kwa mujibu wa Sheria Sura 448 imeona iangalie kwa upya Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ili kuweka Mikakati ya kuitekeleza na hatimaye kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na Mpango wa Shule salama.

Naye Kamishna wa TSC, Jane Mtindya amesema kuwa katika jamii ya sasa ya utandawazi, taarifa zinaenea kwa kasi zaidi tofauti na miaka ya nyuma hivyo ni vyema kuwakumbusha walimu wetu ili wawasaidie kuwa na tabia ya kuzingatia mambo yenye tija kwao na kwa taifa badala ya kuiga tabia ambazo ni kinyume na maadili ya Kitanzania.

"Katika dunia tunamoishi taarifa zinasambaa kwa kasi sana na cha kusikitisha taarifa mbaya zilizo kinyume na maadili yetu ndizo zinazo samba zaidi hususani kwa vijana. Hivyo, kazi hii ya kufafanua Kanuni za Maadili na utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ni muhimu katika kuwasaidia walimu wafanye wajibu wao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuwalea wanafunzi katika maadili mema," alisema.



*Mwenyiki wa TSC, Prof. Willy Komba akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi walioshiriki kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kupitia Rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pichani, aliyekaa upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na kushoto ni mmoja wa Makamishna wa TSC, Jane Mtindya.*



*Mwenyiki wa TSC, Prof. Willy Komba akiwa katika picha ya pamoja na Walimu walioshiriki kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kupitia Rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pichani, aliyekaa upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na kushoto ni mmoja wa Makamishna wa TSC, Jane Mtindya*



*Mwenyiki wa TSC, Prof. Willy Komba akiwa katika picha ya pamoja na washiriki kutoa Wizara na Taasisi mbalimbali walioshiriki kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro hivi karibuni kwa lengo la kupitia Rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Pichani, aliyekaa upande wa kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na kushoto ni mmoja wa Makamishna wa TSC, Jane Mtindya.*



*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Fatma Muya akitoa muhutasari wa rasimu ya ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu wakati wa Kikao kazi kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.*

# WAZAZI/WALEZI MKOANI SIMIYU WAHIMIZWA KUPELEKA SHULE WATOTO WALIOFAULU KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA

**Na Mwandishi Wetu - Simiyu.**

Wazazi na walezi mkoani Simiyu, wametakiwa kupeleka watoto Shule ambao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa Mwaka wa masomo 2023.

Hayo yamesemwa na Katibu Tawala msaidizi anayeshughulikia elimu na mafunzo ya ufundi Mkoa wa Simiyu ambaye pia ni Afisa elimu mkoani humo, Majuto Njanga wakati akizungumza katika kikao kazi cha mapitio ya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu Mkoa wa Simiyu.

Njanga alisema Wanafunzi 32,814 katika wiki ya kwanza walioripoti ni Wanafunzi 7,272 sawa na asilimia 22.7 ya Wanafunzi wote waliochaguliwa.

"Kazi kubwa tunayofanya ni kuhamasisha jamii kuhakikisha wanafunzi wote ambao wamechaguliwa wanafika shule kwa muda unaotakiwa na tayari tumetoa taarifa kupitia vyombo vinavyohusika kwa kushirikisha vyombo vya ulinzi, Serikali za kijiji na kata kuhakikisha watoto wanafika shule.

"Tunataka watoto wote pasiwe na changamoto itakayokuwa inamzuia…kama ni suala la sare za shule hana aende na zile za msingi wakati wazazi/walezi wanaendelea kuwajibika kuwatafutia…tunatoa rai wale wote ambao wataonekana wanasita pasipo na sababu kuwapeleka watoto shule basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa sheria ya elimu no 25 ya mwaka 1978 ambayo inasomeka katika sura 353 kifungu cha 35 (1) ambacho kinahitaji mwanafunzi aweze kuandikishwa katika masomo ambayo anaendelea nayo pasiwe na mtu ambaye anaweza kuzuia kuhakikisha anapata haki yake ya elimu," amesema Njanga.



*Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange (wan ne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto), Watumishi wa TSC pamoja na wadau wengine wa elimu kutoka Mkoa wa Simiyu.*

Alisema suala hilo si kwa shule za Sekondari ni pamoja na watoto ambao hawajaandikishwa elimu ya awali kwamba wanatakiwa waweze kwenda shule na umri wa kwenda darasa la kwanza wapelekwe shule.

Mwakilishi wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Suzana Nussu alisema Mkoa huo unatakiwa kuchukua hatua za madhubuti ili uweze kufanya vizuri kitaalam kwani kwa sasa umeshuka ambapo ametaka kupitia kikao hicho kutoa namna bora ya kutoka walipo na kusonga mbele.

Kwa upande, Paulina Nkwama ambaye ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) alisema ni vema kuhakikisha wanafunzi wanamaliza mzunguko ikiwa sambamba na kuhakikisha wanafunzi wanaoandikishwa kujiunga na elimu ya awali na

# WAZAZI/WALEZI MKOANI SIMIYU WAHIMIZWA KUPELEKA SHULE WATOTO WALIOFAULU KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA

darasa la kwanza ikiwa sambamba waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanaripoti shule.

“Haya tusiyachukue kwa wepesi, kati ya vitu vya msingi ambavyo tunapaswa kuvisisitiza ni swala la uandikishaji wa elimu ya awali, darasa la kwanza na kuhakikisha kidato cha kwanza wanaripoti… kingine tuhakikishe tunaondoa mdondoko wa wanafunzi, Kitaifa ni 0.8 iliyokuwepo mwanzo imepanda hadi 1.8 kwahiyo imeongezeka kwa kiwango kikubwa tunapaswa kuhakikisha wale wanaokuja shule wanakuwepo shule na tunawasimamia hadi wamalize mzunguko.”

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange amewataka wazazi wote wenye watoto wanaopaswa kwenda shule kuwapeleka shuleni mara moja.

“Mkoa huu (Simiyu) ni wa kichungaji wanaamini kwamba mtoto akienda kuchunga mifugo anakuwa amefanya tija ndani ya familia/ familia wanaamini kwamba wakiozesha mtoto wa kike ng’ombe 20 wanakuwa wamefaidika ndani ya jamii sasa sisi mkoa wa Simiyu hatukubaliani na hili Hakuna mwanafunzi ambaye hatohudhuria darasani wanafunzi wote waliofaulu wanatakiwa kuwa shule. Walimu wetu wana utayari wa kufanya kazi, Mheshimiwa Rais ametujengea madarasa 239 mkoani kwetu, wote waliofaulu waende shule,” alisema Kapange.

Neema Makundi ambaye ni Afisa Elimu Taluma wa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa alisema wapo tayari kuyatekeleza yote waliyoagizwa kuyafanya katika kikao hicho.




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu katibu Wasaidizi wa TSC wa wilaya za Mkoa wa Simiyu.*

# TSC NGORONGORO YATEMBELEA SHULE YA SEKONDARI SOITSAMBU

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ngorongoro ikishirikiana na Chama cha Walimu Tanzania (CWT), imefanya ziara katika shule ya Sekondari Soitsambu, kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu wa shule hiyo juu ya masuala mbalimbali ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu.




*Picha ya pamoja kati wa Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Ngorongoro, Bahati Mzirai, Katibu wa CWT Wilaya ya Ngorongoro pamoja na walimu wa shule ya Sekondari Soitsambu.*











*Kikao cha TSC Wilaya ya Ngorongoro na walimu wa shule ya Sekondari Soitsambu kikiwa kinaendelea.*

# BENKI YA DUNIA YAONESHA KURIDHISHWA NA TSC KATIKA KUTEKELEZA KAZI ZA MRADI WA BOOST

**Na Mwandishi Wetu – Morogoro.**



*Mwakilishi wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Gema Toddy akiwa katika kikao kazi cha wadau wa elimu waliokutana mjini Morogoro Januari 10 – 13, 2023 kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu.*

Benki ya Dunia ambayo ni mfadhili wa Mradi wa BOOST imeonesha kuridhishwa na namna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inavyotekeleza moja ya malengo ya mradi huo katika kuwasaidia walimu kuwa na mwenendo mwema unaozingatia miiko na maadili ya kazi hiyo.

Hayo yameelezwa na Mtaalamu wa Elimu kutoka Benki ya Dunia ambaye pia ni Msaidizi Mkuu wa Mradi wa BOOST, Gemma Todd wakati wa Kikao kazi kilichoandaliwa na TSC kwa lengo la kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika Januari 10 – 13, 2023 mjini Morogoro.

Amesema kuwa Mradi wa BOOST unalenga kuimarisha na kuboresha elimu ya Awali na Msingi kwa shule za Serikali ambapo shughuli mbalimbali zimepangwa kuanyika ili kufikia lengo hilo, shughuli hizo ni kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, kuhakikisha shule zina usalama wa kutosha, kujenga shule mpya na madarasa mapya na kuhakikisha walimu wanapata mafunzo mara kwa mara na kwa karibu.

"Nimeshiriki kwenye warsha nzuri sana ambayo imeandaliwa na TSC kujadili maadili ya walimu wetu, tunajua watoto watashidwa kusoma wasipokuwa na usalama shuleni, pia wasipokuwa na walimu ambao wanaweza kuwa karibu nao na kuweza kuwaongoza vizuri. Kwa kweli warsha hii imekwenda vizuri na matokeo ya warsha hii ni kutusaidia kufikia malengo ya afua namba mbili ya mradi wetu ambayo inazungumzia shule salama", alisema Todd.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akisalimiana na Mwakilishi wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Gema Toddy mjini Morogoro katika kikao kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu.*

Ameeleza kuwa katika mazingira ya sasa ambapo kumekuwa na mabadiliko ya kitabia yanayosababisha kuharibika kwa maadili katika jamii ni muhimu kuweka mkazo katika kusaidia walimu kuzingatia Miiko na Maadili ya kazi yao ili kufanya shuleni kuwa mahali salama kwa wanafunzi, hivyo TSC imefanya jambo la msingi sana kwa kuamua kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Maadili na Utendaji kazi wa Walimu.

# BENKI YA DUNIA YAONESHA KURIDHISHWA NA TSC KATIKA KUTEKELEZA KAZI ZA MRADI WA BOOST

"Kanuni za Maadili hayo zikifafanuliwa vizuri na kueleweka zitamwongoza mwalimu kutambua wajibu wake awapo shuleni au eneo lake la kazi kwa kuwa wajibu wake ni zaidi ya kufundisha darasani. Mwalimu anawajibika katika malezi ya mtoto kimwili, kiakili, kiroho, kijamii na kisaikolojia. Lakini pia ana wajibu kwa viogozi wake na wasimamizi wake wa kazi, anawajibika kwa jamii anamoishi na anawajibika kwa Umma au Taifa kwa ujumla. Haya yote yamejadiliwa kwa kina katika warsha hii," alisema Todd.

Todd amefafanua kuwa pamoja na wajibu, walimu kama watumishi wengine wana haki zao ambazo ni lazima zilindwe na kutetewa ili watekeleze majukumu yao katika mazingira ya amani, furaha na utulivu, hivyo ni wajibu wa TSC pamoja na mamlaka zingine zinazosimamia walimu kuwaelimisha juu ya haki hizo ili waweze kuwajibika vizuri.



*Mwakilishi wa Mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Gema Toddy (kushoto) akiwa na Mratibu wa Mradi huo kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Neema Lemunge wakati wa kikao kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika Januari 10 – 13, 2023 mjini Morogoro.*

Mradi wa BOOST unafuata utaratibu wa lipa kutokana na matokeo, ikimaanisha kuwa kila mwaka Benki ya Dunia itukakaa na Serikali kupitia Wizara na Taasisi zinazotekeleza mradi huo kwa ajili ya kupima matokeo ya kazi zilizofanyika, hivyo fedha za mwaka unaofuata zitatolewa endapo matokeo ya upimaji huo yataonesha malengo yanatekelezwa vizuri.

"Tuna imani kubwa kwa namna TSC inavyotekeleza sehemu ya mradi huu na ni matumaini yetu kuwa matokeo ya hiki kinachofanyika nikuona walimu wakifanya kazi zao kitaaluma na kitaalam ili wanafunzi wapate ujuzi katika masomo yao lakini wawe mfano wa kuigwa kwa kuwa na maadili mema kwa jamii na Taifa kwa ujumla," alisema Todd.

Alimema kuwa mradi wa BOOST unatekelezwa na Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) na kueleza kuwa Taasisi zilizo chini ya Wizara hizo zinazotekeleza mradi huo ni TSC, Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani Tanzania pamoja na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*

# BENKI YA DUNIA YAONESHA KURIDHISHWA NA TSC KATIKA KUTEKELEZA KAZI ZA MRADI WA BOOST

Naye Mkurugezi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Bi. Fatma Muya amesema kuwa TSC iliandaa andiko la Mradi ambalo lilikubalika na kupata ufadhili ambapo alieleza kuwa moja ya kazi zilizokubalika kutekelezwa katika mradi huo ni kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ambazo walimu wanapaswa kuzitekeleza ili kuboresha elimu na kuwa na shule salama.

"Kwa sasa tupo katika hatua ya kuandaa ufafanuzi huo na kwenye kikao kazi hiki tumewaita wadau mbalimbali waliobobea katika masuala ya elimu na Walimu wakiwemo Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Elimu, Haki Elimu, Taasisi ya Elimu, ADEM, Taasisi ya Elimu Tanzania, Chuo Kikuu Dodoma, Chama cha Walimu Tanzania pamoja na wadau wengine waliobobea katika utumishi wa Walimu," alisema Muya.



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*

Amefafanua kuwa kazi inayofanyika katika kikao kazi hicho ni kupitia na kuboresha rasimu ya Mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu ambayo iliandaliwa na Menejimenti ya Tume hiyo na baada ya kikao kazi hicho, hatua itakayofuata ni kuchapisha na kusambaza vitabu shuleni pamoja na kutoa elimu kwa wadau mbalimbali.



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kushoto) akijadiliana jambo na mmoja wa Makamishna wa Tume hiyo, Jane Mtindya wakati wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023.*

Ameongeza kuwa TSC inatarajia kwamba ufafanuzi huo utasomwa na kueleweka kwa walimu wote kwa kuwa umeandikwa katika lugha rahisi na kutoa elimu kwa wadau juu ya Kanuni hizo, hivyo kila mwalimu ataelewa misingi ya kile anachopaswa kufanya katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi huo kwa upande wa TSC, Bi. Neema Lemunge amesema kuwa pamoja na kazi ya kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili katika Utumishi wa Walimu, Mradi wa BOOST umefadhili utekelezaji wa shughuli zingine ikiwemo kufanya mapitia ya Sheria mbalimbali zinazohusu walimu, ununuzi wa vitendeakazi vikiwemo magari na kompyuta.



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*



*Washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023 wakiwa katika vikundi kwa ajili ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo na kuiboresha.*



Mwenyekiti wa Kikao wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023, Wakili Richard Odongo akizungumza na washiriki (hawapo pichani) wa kikao kazi hicho juu ya namna ya kupitia rasimu ya ufafanuzi huo kipengele kwa kipengele.



Makamu mwenyekiti wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023, Dkt. Fidel Dassan Gwajekera akiongoza washiriki (hawapo pichani) katika kujadili rasimu ya Ufafanuzi huo.



Mmoja wa washiriki wa Kikao Kazi cha kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro Januari 10 -13, 2023, akichangia hoja kwa ajili ya kuboresha rasimu ya Ufafanuzi huo.




# MAAFISA BAJETI TSC WAANDAA MAOTEO YA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024




*Maafisa Bajeti wa TSC, wakiwa katika kikao cha kuandaa Maoteo Bajeti ya TSC kwa mwaka 2023/2024 kilichofanyika mjini Singida hivi karibuni.*



*Mtumishi wa TSC, Damas Mapunda (kushoto) akimuonesha jambo Ramadhan Ngaegela wakati wa kikao cha Maafisa Bajeti cha kuandaa Maoteo Bajeti ya TSC kwa mwaka 2023/2024 kilichofanyika mjini Singida hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC, Patory Munyaki (kushoto) na Frenki Makundi wakijadiliana jambo wakati wa kikao cha Maafisa Bajeti cha kuandaa Maoteo Bajeti ya TSC kwa mwaka 2023/2024 kilichofanyika mjini Singida hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC, Elia Malaki (kushoto) na Timoth Mtafya wakiendelea na kazi wakati wa kikao cha Maafisa Bajeti cha kuandaa Maoteo Bajeti ya TSC kwa mwaka 2023/2024 kilichofanyika mjini Singida hivi karibuni.*



*Watumishi wa TSC, Francis Gwankisa (kushoto) na Fundikira James wakijadiliana jambo wakati wa kikao cha Maafisa Bajeti cha kuandaa Maoteo Bajeti ya TSC kwa mwaka 2023/2024 kilichofanyika mjini Singida hivi karibuni.*

# WATUMISHI TSC WAKATA KEKI KUUKARIBISHA MWAKA 2023




*Keki iliyoandaliwa na Watumishi wa TSC kwa ajili ya kuukaribisha mwaka 2023.*





*Watumishi wa TSC wakiwa katika hafla fupi ya kuukaribisha mwaka 2023 iliyofanyika TSC Makao Makuu Dodoma mapema mwezi Januari, 2023.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akikata keki ikiwa ni ishara ya kuukaribisha mwaka 2023.*



*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Zachary Dida akitoa salamu za mwaka mpya kwa watumishi wa TSC.*

# WATUMISHI TSC WAKATA KEKI KUUKARIBISHA MWAKA 2023











*Katibu wa TSC akiwalisha keki watumishi mbalimbali wa TSC.*

# WATUMISHI TSC WAKATA KEKI KUUKARIBISHA MWAKA 2023





*Katibu wa TSC akiwalisha keki watumishi mbalimbali wa TSC.*



*Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Fatuma Muya (kushoto) akifurahia jambo na Mkurugenzi Msaidizi Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mecktildis Kapinga wakati wa hafla fupi ya kuukaribisha mwaka 2023 iliyofanyika TSC Makao Makuu Dodoma mapema mwezi Januari, 2023.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza kikao cha Menejimenti ya TSC kujadili Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu. Kikao hicho kilifanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Fatuma Muya akitoa ufafanuzi juu ya Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu katika kikao cha Mejenimenti ya TSC kilichofanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma.*



*Mkurugeni wa Idara ya Huduma za Sheria wa TSC, Wakili Richard Odongo akitoa ufafanuzi wa masuala ya kisheria wakati wa kikao cha Menejimenti ya TSC kilichifanyika kwa ajili ya kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu. Kikao hicho kilifanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma.*



*Mratibu wa Mradi wa BOOST kutoka TSC, Mwl. Neema Lemunge akitoa maelezo ya Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kwenye Kikao cha Menejimenti cha TSC kilichofanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma. Mradi wa BOOST ndio waliofadhili uandaaji wa Ufafanuzi wa Kanuni hizo.*



*Wajumbe wa Kikao cha Menejimenti cha TSC wakiwa kwenye kikao cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu. Kikao hicho kilifanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma.*



*Wajumbe wa Kikao cha Menejimenti cha TSC wakiwa kwenye kikao cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu. Kikao hicho kilifanyika mapema mwezi Januari, 2023 jijini Dodoma.*

# "ZINGATIENI TARATIBU KUTOA ADHABU YA VIBOKO MASHULENI" - WAZIRI KAIRUKI

**Na. Mwandishi Wetu – Dar Es Salaam.**



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Angellah Jasmine Kairuki, amewataka Walimu wote kote nchini kufuata taratibu zilizoainishwa kwenye Waraka Namba 24 wa Mwaka 2002 ambao umeeleza wazi ni nani mwenye mamlaka ya kutoa adhabu ya viboko na viboko vingapi vinaruhusiwa nakwa utaratibu upi vinatolewa kwa wanafunzi.

Waziri Kairuki aliyasema hayo Jijini Dar Es salaam hivi karibuni wakati akizungumza na Maafisa Elimu Kata, Wakuu wa Shule za Sekondari, Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Viongozi wa Elimu ngazi ya Halmashauri kwenye Kikao Kazi cha Uboreshaji wa Usimamizi wa Elimu Msingi na Sekondari katika Jiji la Dar es Salaam.

"Suala zima la adhabu ya viboko mashuleni linaongozwa na Waraka wa Elimu Namba 24 wa Mwaka 2002 na umeeleza bayana kabisa." Alisema Waziri Kairuki

Waziri huyo aliendelea kufafanua kuwa Waraka huo na Kanuni zake za Elimu za Mwaka 2002 ni lazima zifuatwe katika utolewaji wa adhabu ya viboko mashuleni kote hapa nchini.

"Kwa mujibu wa Mwongozo huo ambao umeelekeza adhabu hiyo ya viboko kuwa inaweza kutolewa pale ambapo umetokea utovu wa nidhamu uliokithiri au makosa ya jinai yaliyotendeka ndani au nje ya shule yenye muelekeo wa kuishushia heshima shule, basi adhabu tajwa katika Mwongozo huo inaweza kutolewa kwa utaratibu ulioelekezwa." Alisisitiza Mhe. Kairuki.

Pia Waziri huyo aliendelea kuelekeza kuwa; "Kwa mujibu wa Waraka huo adhabu hiyo inavyotolewa lazima izingatie vigezo ikiwemo ukubwa wa kosa, umri wa mwanafunzi, jinsi na afya ya mtoto na haipaswi kuzidi viboko vinne kwa wakati mmoja."

Alieleza kuwa, Waraka huo umeelezea namna adhabu hiyo inapaswa kutolewa kwa mtoto wa jinsia ya kike na kwa mtoto jinsia ya kiume ikiwa kwa mtoto jinsia ya kike inapaswa adhabu kutolewa mikononi, nakwa



# "ZINGATIENI TARATIBU KUTOA ADHABU YA VIBOKO MASHULENI" - WAZIRI KAIRUKI

mtoto wa jinsia ya kiume adhabu inapaswa kutolewa makalioni.

Pia, Waziri Kairuki alibainisha kuwa Waraka huo umeeleza wazi kuwa mwenye dhamana na mamlaka ya kutoa adhabu ya viboko ni Mwalimu Mkuu au Mkuu wa Shule husika au Mwalimu mwingine atakayekuwa ameteuliwa tena awe ameteuliwa kwa maandishi.

Vilevile, Waziri huyo wa TAMISEMI alitanabaisha kuwa kwa mtoto wa kike imeelekezwa aadhibiwe na Mwalimu wa kike au labda tu kama shule hiyo husika haina mwalimu wa kike ndipo anaweza kuadhibiwa na Mwalimu wa kiume.

Waziri Kairuki alitoa rai kwa Walimu wote nchini kukumbuka kuwa wamekasimiwa dhamana na mamlaka ya kuwa walezi na walinzi wa watoto wanapokuwa shuleni kwahiyo wasiwe sehemu ya kuwafanya watoto kuwa watoro kupitia adhabu wanazozitoa zinazokiuka kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali zilizowekwa.






"Hatusemi watoto wasichapwe lakini wachapwe kwa kufuata taratibu na vigezo nakwa mujibu wa miongozo na taratibu zilizowekwa." Alisisitiza Waziri Kairuki.



Pamoja na hayo aliwaonya Walimu wote nchini watakaoendelea kukiuka Kanuni, Mwongozo na Taratibu hizo kuwa hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Walimu na Umma kwa ujumla.

# DKT. MSONDE: TSC, MAAFISA ELIMU, WATHIBITI UBORA WA SHULE HAKUNA KUKAA OFISINI




*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akiongea wakati wa kuhitimisha kikao kazi kilichowakutanisha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC (hawapo pichani) kutoka ofisi za Wilaya kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa neno la kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde wakati wa kuhitimisha kikao kazi kilichowakutanisha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka ofisi za Wilaya kilichofayika hivi karibuni mjini Morogoro.*

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ngazi ya Wilaya wametakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Maafisa Elimu pamoja na Wathibiti Ubora wa Shule ili kuweza kutoa huduma bora kwa walimu huku wakitakiwa kuwafuata walimu shuleni badala ya kukaa ofisini kusubiri walimu wapeleke shida zao.

Hayo yamesemwa mwishoni mwa wiki na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde wakati wa kuhitimisha kikao kazi kilichowakutanisha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya zote za Tanzania Bara kilichofanyika mjini Morogoro.

Dkt. Msonde amefafanua kuwa mkakati wa Serikali ni kuhakikisha walimu wanahudumiwa wakiwa shuleni, hivyo TSC, Maafisa Elimu na Wathibiti Ubora wa Shule wanatakiwa kufanya ziara shuleni siku tatu kila wiki na siku mbili pekee ndizo wanazotakiwa kubaki ofisini.

"Serikali haitaki mwalimu aje kutafuta huduma ofisini kwako, ninyi ndio mnapaswa kwenda shuleni kutatua changamoto zao. Kuanzia sasa tumeachana na utaratibu wa zamani wa mwalimu kuja ofisini kupiga magoti akitafuta huduma. Tunataka mwalimu afanye kazi




*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (katikati) akiimba wimbo pamoja na washiriki (hawapo pichani) wa kikao kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.*

# DKT. MSONDE: TSC, MAAFISA ELIMU, WATHIBITI UBORA WA SHULE HAKUNA KUKAA OFISINI



*Mmoja wa washiriki wa Kikao Kazi cha Makatibu Wasaidizi kutoka Ofisi za Wilaya 139 za TSC, Rhoda Mwasulende akitoa neno la shukrani kwa Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde wakati wa kuhitimisha kikao kazi hicho kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

yake ya kufundisha tu, hayo mambo mengine ya madaraja, likizo, nk sisi tuliopewa dhamana ya kuwaratibu ndio tunatakiwa tuyafanye," amesema Msonde.

Kiongozi huyo ameongeza kuwa anatambua kuwa ofisi za TSC ngazi ya wilaya zinakabiliwa na changamoto ya vyombo vya usafiri, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kushindwa kutembelea walimu shuleni kwa kuwa Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu wana magari, hivyo amewataka kuhakikisha wanapanga ratiba ya kutembelea walimu kwa pamoja.

"TSC, Maafisa Elimu na Wathibiti Ubora wa Shule lazima muelewe kwamba, shamba lenu ni kwa walimu ambao wapo shuleni. Hata kama kuna changamoto ya usafiri ni lazima tufanye kila linalowezekana kumfikia mwalimu alipo. Ndiyo maana tumeagiza maafisa elimu wote wanapopanga ratiba zao kwenda shuleni lazima ziendane na ratiba zenu ili mfanye ziara pamoja. Kila mmoja anatakiwa kujua kuwa ana mchango katika kuleta maboresho ya elimu katika Taifa hili, mmoja anaposhidwa kutekeleza wajibu wake maana yake ni kwamba tumeshindwa wote," amesema.

Msonde amesisitiza kuwa hadhi na heshima ya mwalimu ni lazima ilindwe na ni marufuku kumnyanyasa mwalimu kwa namna yoyote ile kwani kufanya hivyo kunamwondolea morali ya kulea wanafunzi kiakili, kimwili, kiroho na kijamii na hivyo kutokea ongezeko la mmomonyoko wa maadili na maendendelo ya elimu kurudi nyuma.

"Lazima tulinde hadhi ya mwalimu, sipendezi kuona au kusikia mwalimu ananyanyaswa. Ndo maana tumesema muwe shuleni kwa siku tatu kila wiki, ofisini tumewaachia siku mbili tu. Muende kuwatia moyo walimu wetu sio muende kukoroma kwa wakuu wa shule, hapana. Mnakwenda shuleni, mshirikiane nao professionally (kitaaluma), muwaone watoto darasani wana mapungufu gani na mkae na walimu kutafuta ufumbuzi kwa pamoja."

Ameongeza kuwa, "Tunataka walimu wetu wajisikie kwamba ni watu wanaohudumiwa na walimu





*Washiriki wa kikao kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro wakisikiliza hotuba ya Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani).*

# DKT. MSONDE: TSC, MAAFISA ELIMU, WATHIBITI UBORA WA SHULE HAKUNA KUKAA OFISINI

wenzao waliopewa dhamana ya kuwaratibu ili nao wajisikie kuwa ni watumishi wanaoheshimiwa," amesema.

Naibu Katibu Mkuu huyo alihitimisha kwa kusema kuwa kufanya kazi kwa bidii na kujituma ni moja ya njia za kuunga mkono juhudi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa kipindi kifupi alichokaa madarakani amefanya mapindizi makubwa katika sekta ya elimu nchini.

"Rais amefanya mambo mkubwa katika kuleta mapinduzi ya elimu, kwa miaka 5 kuanzia mwaka 2021 kiasi cha shilingi trilioni 1.2 kinaendelea kutumika kujenga shule 1026 za Sekondari. Kwenye shule za Msingi kupitia Mradi wa BOOST kiasi cha shilingi trilioni 1.15 zitatumika kwa ajili ya kuimarisha elimu ikiwemo ujenzi wa shule mpya, ukarabati wa shule, ujenzi wa madarasa, pamoja na kuendeleza utumishi wa walimu ambapo TSC ni miongoni mwa wanufaika katika mradi huo.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amesema kupitia Mradi wa BOOST TSC imeweza kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ambapo imeandaa kitabu cha ufafanuzi huo kitakachosambazwa shuleni ili kuwafanya walimu watekeleze wajibu wao kwa kuzingatia miiko na taratibu za kazi hiyo.

Amesema kikao kazi hicho kilichofanyika kwa siku nne kuanzia Januari 24 – 27, 2023 pamoja na mambo mengine, kilikuwa cha mafunzo kwa Kaimu Katibu Wasaidizi 139 wa kuhusu ufafanuzi wa Kanuni hizo ambao nao watakwenda shuleni kutoa elimu hiyo kwa walimu.







*Washiriki wa kikao kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro wakisikiliza hotuba ya Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde (hayupo pichani).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Menejimenti ya TSC wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Mashariki wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Kusini wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Kati wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa Wilaya kutoka Kanda ya Ziwa wakati wa uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*



*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Mhe. David Silinde (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Sekretarieti ya uzinduzi wa Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliofanyika Januri 24, 2023 mjini Morogoro. Pichani, kwa waliokaa ni Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba (wa pili kutoka kushoto) na Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia).*

# TSC YATAKIWA KUONGEZA JUHUDI KUSIMAMIA MAADILI NA MSAWAZO WA WALIMU NCHINI

**Na Mwandishi wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetakiwa kuhakikisha inasimamia kwa karibu maadili na nidhamu ya walimu pamoja na kuhakikisha uwepo wa msawazo sawa wa walimu kwa shule za mijini na za vijijini ili kuharakisha maendeleo ya elimu nchini.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Ally Musa kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) wakati wa kufunga kikao kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka katika ofisi 139 za wilaya pamoja na Menejimenti ya Tume hiyo.

Kikao kazi hicho kilichofanyika kwa siku nne mjini Morogoro pamoja na mambo mengine kililenga kuwajengea uwezo




*Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Ally Musa akifunga kikao kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka katika ofisi 139 za wilaya pamoja na Menejimenti ya TSC (hawapo pichani) kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro. Katibu Tawala huyo alifunga kikao kazi hicho kwa niaba ya Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI).*

Kaimu Katibu Wasaidizi hao juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu uliotolewa hivi karibuni na TSC kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa BOOST.

Akizungumzia kuhusu ukiukwaji wa Maadili ya Ualimu, Katibu Tawala huyo amesema kuna baadhi ya walimu ambao




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Palina Nkwama akitoa neno la kumkaribisha Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Ally Musa kwa ajili ya kufunga kikao kazi kilichowakutanisha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka katika ofisi 139 za wilaya pamoja na Menejimenti ya TSC. Kikao kazi hicho kilifanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Zachary Dida akitoa utambulisho wakati wa kufunga kikao kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka katika ofisi 139 za wilaya pamoja na Menejimenti ya TSC (hawapo pichani) kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

# TSC YATAKIWA KUONGEZA JUHUDI KUSIMAMIA MAADILI NA MSAWAZO WA WALIMU NCHINI




*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Fatuma Muya akitoa maelezo kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro juu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu yaliyotolewa kwenye kikao kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka katika ofisi 139 za wilaya pamoja na Menejimenti ya TSC (hawapo pichani) kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

wanajipamba kupita kiasi jambo ambalo linasababisha wanafunzi badala ya kuzingatia masomo Huishia kuangalia mapambo ya mwalimu kitu ambacho pamoja na kuwa kinarudisha nyuma maendeleo ya taaluma kwa wanafunzi, kinaondoa hadhi na heshima ya walimu.

"Mkemee masuala ya nidhamu, ninyi ndio wasimamizi wa nidhamu katika shule zetu. Kuna vitendo vinafanyika shuleni ambavyo vinaondoa hadhi ya mwalimu. Unakuta mwalimu amejipamba kupitiliza, usoni, mdomoni, machoni amepaka vitu kupitiliza, wengine pua zimetobolewa zimewekwa urembo mwingi. Mapambo haya yanaweza kumfanya mwanafunzi badala ya kusikiliza masomo akawa anamuangalia mwalimu tu, huo nao ni utovu wa nidhamu," Katibu Tawala huyo amesema.

Ameongeza kuwa changamoto nyingine ya nidhamu ni utoro wa walimu ambapo ameeleza kuwa bado kuna walimu wanaoondoka kwenye vituo vyao vya kazi bila taarifa na wengine wanafika shuleni lakini wanakuwa watoro wa vipindi vyao vya kufundisha.

Amesema utoro wa walimu umesababisha wanafunzi kutomaliza masomo yao ya muhula jambo ambalo linamnyima mwanafunzi haki yake ya kufundishwa na hivyo kurudisha nyuma jitihada za kuleta maendeleo katika sekta ya elimu.

Kiongozi huyo pia, ameitaka TSC kusaidia kuzuia vitendo vya



*Washiriki wa kikao kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kutoka ofisi za Wilaya 139 wakimsikiliza Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Ally Musa (hayupo pichani) wakati wa kufunga kikao kazi hicho kilichofanyika kwa siku nne mjini Morogoro hivi karibuni.*

# TSC YATAKIWA KUONGEZA JUHUDI KUSIMAMIA MAADILI NA MSAWAZO WA WALIMU NCHINI







*Washiriki wa kikao kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kutoka ofisi za Wilaya 139 wakimsikiliza Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Musa Ally Musa (hayupo pichani) wakati wa kufunga kikao kazi hicho kilichofanyika kwa siku nne mjini Morogoro hivi karibuni.*

udhalilishaji vinavyofanywa kwa wanafunzi ikiwemo uhusiano wa kimapenzi, ubakaji, ulawiti, unyanyasaji pamoja na kuadhibu wanafunzi kinyume na taratibu huku akifafanua kuwa vitendo hivyo vinafanywa na baadhi ya walimu na vingine vinafanywa na watu wengine wa mitaani.

"Vitendo vya uzalilishaji, ubakaji, ulawiti, adhabu zisizozingatia taratibu bado vinaendelea kuripotiwa dhidi ya wanafunzi. Inawezekana ubakaji unafanyika nje ya shule lakini bado wapo walimu ambao wanajihusisha na vitendo vya udhalilishaji wa wanafunzi. Na hapa sio kwamba walimu wa kiume tu ndio wanaowafanyia wanafunzi wa kike, lakini siku hizi wapo walimu wa kiume wanawafanyia wanafunzi wa kiume, pia wapo walimu wa kike wanawafanyia wanafunzi wa kiume."

"Tukiweza kudhibiti vitendo hivyo, sekta yetu ya elimu itaendelea kukua na kufikia katika vile viwango tunavyovitaka. Kwa hivyo, Tume mna jukumu kubwa sana kuhakikisha mnaendelea kutoa elimu kuzuia haya yasitokee. Lakini pale inapohitajika chukueni hatua bila kuchelewa ili tuwanusuru watoto wetu," alisema Katibu Tawala huyo.

Vilevile, ameishauri Tume hiyo, kuhakikisha inatekeleza jukumu lake la kuhakikisha msawazo sawa wa walimu kwa shule za mijini na vijijini kwa kuwa kuna wimbi kubwa la walimu wanaotaka kuhama kutoka shule za vijijini kwenda shule zilizopo mijini kitu

# TSC YATAKIWA KUONGEZA JUHUDI KUSIMAMIA MAADILI NA MSAWAZO WA WALIMU NCHINI

ambacho kinasababisha kudorora kwa elimu katika Halmashauri zilizoko pembezoni.

"Katika Mkoa wangu wa Morogoro ninapata maombi mengi ya walimu wanaotaka kuhamia Morogoro Manispaa. Na mimi nimekataa kuruhusu walimu kuhamia Manispaa. Tume ninawasihi tekelezeni jukumu hili ipasavyo, tukiacha hali hii iendelee tutadhoofisha maeneo mengine na kusababisha elimu kudorora kwa kuwa hayatakuwa na walimu wa kutosha kuweza kuhudumia wanafunzi," amesema.

Akitoa neno la kumkaribisha Katibu Tawala huyo, Katibu wa TSC, Mwl. Palina Nkwama amesema kikao kazi hicho kimefanyika kwa lengo la kuwajengea uwezo washiriki ili kuwawezesha kwenda kutoa mafunzo kwa walimu ngazi ya shule kuhusu Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ikiwa ni sehemu ya kuimarisha Maadili na uwajibikaji kwa walimu.

"Mafunzo haya yamehudhuriwa na jumla ya washiriki 170 wakiwemo wajumbe wa Menejimenti ya TSC Makao Makuu (11), Watumishi wa Tume Makao Makuu (20) pamoja na Kaimu Makatibu Wasaidizi kutoka ofisi zote za Wilaya 139," amesema Nkwama.

Aliongeza kuwa mada zilizowasilishwa katika kikao kazi hicho ili washiriki hao waweze kutoa elimu kwa walimu katika ngazi ya shule ni: Mwenendo na Tabia njema ya mwalimu, wajibu wa mwalimu kwa mwanafunzi, wajibu wa mwalimu kwa taaluma yake, wajibu wa mwalimu kwa mkuu wake wa shule, wajibu wa mwalimu kwa watumishi wenzake, wajibu wa mwalimu kwa mwajiri wake, wajibu wa mwalimu kwa jamii, wajibu wa mwalimu kwa Taifa pamoja na ushiriki wa mwalimu katika siasa.

Kwa mujibu wa Nkwama, washiriki hao walipewa maelezo kuhusu ukiukwaji wa Kanuni za Maadili na Utendaji katika Utumishi wa Walimu na adhabu zinazoweza kutolewa dhidi ya ukiukwaji huo.

Mafunzo hayo yamefanyika kwa ufadhili wa banki ya Dunia kupitia mradi wa BOOST ikiwa ni sehemu ya mpango wa kuwa na Shule Salama.



*Mratibu wa Mradi wa BOOST kwa upande wa TSC, Mwl. Neema Lemunge (kulia) akiwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali wa TSC, Gerard Chami wakati wa kufunga Kikao Kazi cha Makatibu Wasaidizi wa TSC kutoka ofisi za Wilaya 139 kilichofanyika hivi karibuni mjini Morogoro.*

# ZIARA YA KATIBU WA TSC IGUNGA NA NZEGA



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye miwani, katikati kwa waliokaa mstari wa katikati) akiwa katika kikao na viongozi wa Elimu (TSC, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu) wa Wilaya ya Igunga katika ziara aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Igunga wakati wa ziara aliyoifanya wilayani hapo hivi karibuni.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC Wilaya ya Nzega wakati wa ziara aliyoifanya wilayani Nzega hivi karibuni.*




*Mkurugenzi wa Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*




*Mkuu wa Kitengo Ununuzi kutoka TSC, Lameck Mbeya akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka TSC, Zachary Dida akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*



*Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA kutoka TSC, Kainda Ndasa akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*




*Mkuu wa Kitengo cha Uhasibu kutoka TSC, CPA Revocatus Misonge akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kutoka TSC, Gerard Chami akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*



*Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini kutoka TSC, Ecodia Pangani akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*



*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kutoka TSC, Thomas Tambilija akiwasilisha mada wakati wa Kikao Kazi cha Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kilichofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.*

# WALIMU MKOANI RUVUMA WATAKIWA KUWEKA MIKAKATI YA KUBORESHA UFUNDISHAJI

**Na Mwandishi Wetu – Ruvuma.**



*Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Dkt. Julias Ningu (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika Kikao Kazi kilichowakutanisha Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisa Elimu na Wakuu wa Shule, wote kutoka Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma kilichofanyika katika Ukumbi wa Shule ya wasichana Songea (Songea Girls) Manispaa ya Songea hivi karibuni. Pichani, wa pili kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama na wa kwanza kutoka kulia ni Kamishna wa TSC na Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mwl. Zusana Nussu.*

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR –TAMISEMI) Angellah Kairuki ametoa maagizo kuhakikisha Walimu wanakuwa na mikakati ya kuboreha ufundishaji kwa wanafunzi Mkoani Ruvuma.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo Dkt Julias Ningu amemwakilisha Waziri huyo katika Kikao Kazi kilichofanyika katika Ukumbi wa Shule ya wasichana Songea (Songea Girls) Manispaa ya Songea na kujumuisha Wakurugenzi wa Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma, Maafisa Elimu na Kuu wa Shule.

Akizungumza katika kikao kazi hicho Ningu amesema kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI amewataka kuandaa mikakati ya ufundishaji itakayosaidia kuleta tija katika Sekta ya Elimu na kuondoa changamoto ya kusababisha dondoko katika Mkoa wa Ruvuma na Nchi nzima .

Amesema kila Afisa Elimu afanye ufuatiliaji angalau kwenye shule mbili kila siku na kushauriana na walimu kikamilifu juu ya namna bora ya kuwafundisha wanafunzi huku akielekeza kuwa walimu wajiwekee malengo binafsi katika masomo wanayofundisha pamoja na kutambuliwa kwa kazi yao kwa kutiwa moyo na kutodhalilishwa na mtu yoyote.

"Kila kiongozi ahakikishe wanafunzi wa Shule za msingi na Sekondari wanakula Shuleni pamoja na kuhakikisha anaimarisha uwajibikaji wa watumishi wote katika ngazi zote ili kuongeza tija katika utendaji kazi," amesema.



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC kutoka wilaya za Mkoa wa Ruvuma.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia kwa waliosimama) akiwa katika picha ya pamoja na Walimu na Wanafunzi wa Shule ya Wasichana Songea (Songea Girls). Pichani, wa kwanza kushoto (waliosimama) ni Kamishna wa TSC na Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mwl. Zusana Nussu.*

# WALIMU MKOANI RUVUMA WATAKIWA KUWEKA MIKAKATI YA KUBORESHA UFUNDISHAJI

Hata hivyo amesema Walimu wanabahati kubwa kwa sababu ni cheo ambacho hakina kustaafu kwa kuwa baada ya kustaafu katika ajira, bado wanaendelea kuitwa walimu.

Naye Ktibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amesema walimu wana wajibu mkubwa kuhakikisha wanafunzi wanapata ujuzi katika taaluma zao pamoja na kuwa na maadili mema katika jamii, hivyo suala la mwenendo mwema unaanzia kwa walimu.

"Mwalimu hawezi kumtengeneza mwanafunzi bora bila yeye kuwa bora kwanza. Hivyo walimu lazima wazingatie miiko na maadili ya utendaji kazi kama inavyoelekezwa katika Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma. Mwalimu anawajibika kulea mtoto kimwili, kiakili, kisaikolojia, kiroho na kijamii.



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Wasichana Songea (Songea Girls) wakiwa darasani.*

Kwa uapnde wake, Naibu Mkurugenzi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka OR - TAMISEMI Suzan Nussu amesema Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa alizindua rasmi miongozo ya usimamizi na utekelezaji wa mikakati ya kuboresha Elimu nchini Agosti 4, 2022 ambayo inalenga kufanya maboresho katika elimu.



*Kamishna wa TSC na Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mwl. Zusana Nussu akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Wasichana Songea (Songea Girls) wakiwa darasani.*

Amesema kupitia mikakati hiyo Waziri wa OR - TAMISEMI ameelelekeza kukutana na wadau wa Elimu ili kuelekezana na kukubaliana namna ya kuongeza kasi katika kutekeleza mikakati hiyo.

"Mheshimiwa Rais ameweka sana katika Sekta ya Elimu tufike mahali tuone jitihada za Rais, tumekuwa tukifanya vizuri lakini yapo maeneo machache yanatukwamisha, hivyo kwa lugha nyingine ya Kikristo kupitia kikao hiki tumebatizwa upya".

# WALIMU MKOANI RUVUMA WATAKIWA KUWEKA MIKAKATI YA KUBORESHA UFUNDISHAJI




*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (wa kwanza kushoto kwa waliosimama) akiwa pamoja na walimu na wanafunzi wa Shule ya Wasichana Songea (Songea Girls) darasani.*



*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Kamishna wa TSC na Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mwl. Zusana Nussu kwenye jiwe la msingi la Shule ya Sekondari ya Wasichana Dkt. Samia Suluhu Hassan iliyopo mkoani Ruvuma inayoendelea kujengwa. Jiwe la Msingi limewekwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Januari 06, 2023.*




*Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika Shule ya Sekondari Nasuli iliyoko mkoani Ruvuma.*

# BOOST INAVYOBORESHA ELIMU YA AWALI, MSINGI NCHINI

**Na Mwandishi wetu- Tanzania.**

Moja kati ya mafanikio tunayoyaona nchini ni kutokana na juhudi za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kutafuta wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuchangia maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Kati ya mafanikio ya miradi ya maendeleo ni pamoja na mradi wa BOOST unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

Boost ni sehemu ya Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu ya awali ya pili (EPforR II) na inachangia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mradi huu umetengewa kiasi cha Sh trilioni 1.15 ambazo zimeelekezwa kwenye sekta ya elimu katika kuboresha elimu ya awali na msingi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais ,Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,(TAMISEMI) Angellah Kairuki, anaeleza haya mjini Morogoro kwenye kikao kazi cha mapitio ya tathimini ya utekelezaji wa shughuli za uboreshaji na usimamizi wa elimu kwa mwaka 2022 na mpango mwaka 2023.

Waziri Kairuki anasema matokeo muhimu ni pamoja na fedha hizo kutumika kujenga vyumba vipya vya madarasa 12,000 na vifaa vya shule vinavyohusika katika maeneo yenye uhitaji zaidi.

Pia kutakuwa na ujenzi wa vituo 800 katika shule za msingi, vituo vya walimu kuanzishwa na kuendelezwa kwa ajili ya utoaji wa mafunzo kwa njia ya TEHAMA kupitia maktaba mtandao "kielekroniki" na mifumo ya usimamizi wa ujifunzaji kimtandao.

Waziri Kairuki anasema shule za msingi 6,000 zitawezeshwa kutekeleza programu ya shule ya msingi salama , madarasa 12,000 ya elimu ya awali yaliyoboreshwa pamoja na njia bora za ufundishaji vikiwemo vifaa vya ujifunzaji.

Eneo lingine la matokeo muhimu ni kuongezeka kwa uwiano wa uandikishaji wanafunzi wa elimu ya awali kutoka asilimia 76.9 hadi kufikia asilimia 85.

Kuongezeka kwa uwiano wa uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali kutoka asilimia 57.5 hadi asilimia 65.6 kwa halmashauri zilizo katika kundi la robo ya chini.

Pia kuongezeka kwa kiwango cha wanafunzi kubaki shuleni katika halmashauri zilizopo katika kundi la robo chini kutoka asilimia 55.9 hadi asilimia 66.24.

Kairuki anasema eneo lingine muhimu ni asilimia 50 ya wanafunzi wa darasa la pili kufikia kiwango cha chini cha kumudu stadi za kusoma na kuandika na asilimia 35 katika kuhesabu.

Ushiriki wa walimu katika mpango wa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kufikia asilimia 50, kuimarisha na kuunganisha mifungo ya Tehama katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji katika shule teule za msingi 800.

Kairuki anasema Mpango wa ujenzi na ukaratabi wa miundombinu ya shule hizo unatarajia kuanza kutekelezwa Januari na Februari mwaka huu (2023) nchini kote.

"Baadhi ya shule zitavunjwa na kujengwa upya, nyingine zitafanyiwa ukarabati mkubwa pamoja na mdogo kwa lengo la kuzifanya ziwe na mazingira bora



*Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

# BOOST INAVYOBORESHA ELIMU YA AWALI, MSINGI NCHINI

kulingana na hali ya sasa kwa walimu na wanafunzi" anasema Kairuki

Kairuki anasema serikali inatambua shule nyingi ni za muda mrefu ambazo zilijengwa na serikali, wadau na wazee na nyingine kwa njia ya kujitolea ambazo zimeweza kudumu kwa muda mrefu na imefika wakati sasa wa kuziboresha.

"Nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mhe Rais kwa jitihada kubwa hizi anazoendelea kuzifanya katika kuimarisha na kuboresha sekta ya Elimu nchini" anasema Kairuki.

Waziri Kairuki anawahimiza watendaji wa sekta ya elimu kuhakikisha wanafunzi wanapata umahiri wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu wamalizapo darasa la kwanza, na kwamba ufundishaji wa somo la Kiingereza unaimarishwa kwa shule za Msingi na Sekondari.

"Kila kiongozi wa elimu katika ngazi ya shule, Kata, Halmashauri na mikoa ahakikishe anafuatilia ufundishaji wa walimu darasani pamoja na kutatua kero za walimu kwenye maeneo yao ya kazi shuleni badala ya kukaa ofisini" anasema Waziri.

Kuhusu uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi nchini anawaagiza watendaji wa sekta ya elimu, wakurugenzi wa halmashauri, wakuu wa wilaya na mikoa kuongeza kasi ya kusajili wanafunzi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya asilimia 100 .

"Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa muendelee kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi wa elimu ya awali na msingi ili kuhakikisha mnafikia malengo ya uandikishaji mliyokuwa mmejiwekea ifikapo muda uliopangwa" anasema Waziri Kairuki.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Angellah Kairuki.*

Waziri Kairuki anasema "Kila kiongozi ahakikishe anaimarisha uwajibikaji wa watumishi wote katika ngazi zote ili kuongeza tija katika utendaji wa kazi" alisisitiza Waziri.

Kairuki anasema Januari 2023 anatarajia kutakuwa na mabadiliko makubwa katika usimamizi wa elimu msingi na sekondari katika shule zetu.

"Kwa msingi huo ni lazima kila mmoja wetu ahakikishe malengo ya serikali ya kuboresha elimu msingi na sekondari yanafikiwa kwa kuwajibika ipasavyo na kutatua changamoto zinazojitokeza " anasema Waziri Kairuki.

Waziri Kairuki anawahimiza Viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri wahakikishe wazazi wanahamasishwa ili kuwezesha wanafunzi kupata chakula cha mchana shuleni.

Naye Mtaalamu wa Elimu kutoka Benki ya Dunia (WB), ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Mradi wa BOOST nchini, Gemma Todd anasema Benki hiyo imeonesha kuridhishwa na namna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inavyotekeleza moja ya malengo ya Mradi huo kuwasaidia walimu kuwa na mwenendo mwema unaozingatia miiko na maadili ya kazi yao.

Todd anaeleza haya kwenye kikao kazi kilichoandaliwa na Tume hiyo, kwa lengo la kufanya mapitio ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu.

"Nimeshiriki kwenye kikao kazi hiki kilichoandaliwa na TSC kujadili maadili ya walimu wetu, tunajua watoto watashidwa kusoma wasipokuwa na usalama shuleni,

# BOOST INAVYOBORESHA ELIMU YA AWALI, MSINGI NCHINI



*Mikutano ya kufanya Maboresho ya Elimu inayofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa BOOST ikiwa inaendelea.*

pia wasipokuwa na walimu ambao wanaweza kuwa karibu nao na kuweza kuwaongoza vizuri" anasema Todd.

"Matokeo ya kikao kazi hiki yatatusaidia kufikia malengo ya afua namba mbili ya mradi wetu ambayo inazungumzia shule salama" anasema Todd.

Todd anasema pamoja na wajibu, walimu kama watumishi wengine wana haki zao ambazo ni lazima zilindwe na kutetewa ili watekeleze majukumu yao katika mazingira ya amani, furaha na utulivu.

Anasema ni wajibu wa TSC pamoja na mamlaka zingine zinazosimamia walimu kuwaelimisha juu ya haki hizo ili waweze kuwajibika vizuri.

Todd anasema mradi wa BOOST unatekelezwa na Wizara mbili ambazo ni Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mbali na wizara hizo pia zipo Taasisi zilizo chini ya Wizara zinazotekeleza mradi huo ambazo ni TSC, Taasisi ya Elimu Tanzania, Baraza la Mitihani Tanzania pamoja na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).

Naye Mratibu wa Mradi huo kwa upande wa TSC, Neema Lemunge anasema Mradi wa BOOST umefadhili utekelezaji wa shughuli zingine ikiwemo kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusu walimu, ununuzi wa vitendea kazi vikiwemo magari na kompyuta.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu kutoka OR – TAMISEMI, Vicent Kayombo anasema utekelezaji wa sera ya elimu bila ada imeongeza idadi ya wanafunzi wanaosailiwa kujiunga elimu ya awali, msingi na sekondari nchini

Kayombo anasema bado zipo changamoto kadhaa ikiwemo kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la bila kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Anasema wanafunzi asilimia 20 wanashindwa kufaulu mtihani wa elimu ya msingi na hivyo kushindwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Kayombo anasema kumekuwepo na idadi ndogo kwa wanafunzi wanaofaulu mtihani wa kidato cha nne kwa daraja la kwanza hadi tatu likiwemo somo la Kiingereza.



*Mtaalamu wa Elimu kutoka Benki ya Dunia (WB), ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Mradi wa BOOST nchini, Gemma Todd.*




*Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu kutoka OR – TAMISEMI, Vicent Kayombo.*

# JAKAYA MRISHO KIKWETE FOUNDATION KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUBORESHA UTOAJI WA ELIMU NCHINI

**Na. Mwandishi Wetu – Dodoma.**



Ofisi ya Rais - TAMISEMI inatarajia kuanzisha ushirikiano na Taasisi ya Jakaya Mrisho Kikwete Foundation (JMKF) unaolenga kuanzisha mpango maalum wa kutoa ajira ya muda mfupi kwa Walimu wa kujitolea watakaofundisha Shule za Msingi za Serikali kwa kipindi kisichopungua miaka miwili.

Ushirikiano huo umejadiliwa hivi karibuni katika kikao cha pamoja kati ya Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya JMKF na Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kilichofanyika jijini Dodoma.

Katika kikao hicho, pamoja na mambo mengine, Mhe. Dkt. Kikwete ameishauri Ofisi ya Rais – TAMISEMI kutengeneza kanzidata ya Walimu wote wanaojitolea nchini na kuandaa muongozo utakaosimamia mchakato wa kuwapata Walimu wa kujitolea na kuratibu maslahi yao.

Mhe. Dkt. Kikwete alielezea utayari wa Taasisi ya JMKF kushirikiana kwa karibu na Serikali katika kutekeleza mpango huo ambao tayari Taasisi hiyo imejipanga kuanza kuutekeleza kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na wadau wengine.

Kupitia kikao hicho, Mhe. Dkt. Kikwete aliiomba Serikali kuweka utaratibu mzuri wa kuwaajiri Walimu wa kujitolea watakaomaliza muda wao wa kujitolea ili kufanya mpango huo kuwa endelevu.

Nae Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Angellah Kairuki alimweleza pia Mhe. Dkt. Kikwete kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI imejipanga vema katika kuboresha sekta





# JAKAYA MRISHO KIKWETE FOUNDATION KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUBORESHA UTOAJI WA ELIMU NCHINI

ya elimu kwa kuanzisha utoaji elimu kidijitali kwa kuanzisha maabara za TEHAMA na Sayansi katika shule zote za Serikali hapa nchini, ambapo kwa kuanzia shule mpya zote zinazojengwa zitakuwa na maabara ya sayansi na zitaunganishwa na mfumo wa 'intaneti' ili kufikia lengo hilo.

Aidha, Waziri Kairuki aliipongeza Taasisi ya JMKF kwa kuanzisha programu ya kutoa elimu kidijitali na kwa kuwa tayari kushirikiana na Serikali katika eneo hilo.

Waziri Kairuki alihitimisha kwa kuishukuru Taasisi ya JMKF kwa jitihada zake za kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita katika kuendeleza na kuboresha Sekta ya Elimu nchini na ameahidi kuwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Taasisi hiyo na wadau wengine wa sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo wanaoiunga mkono Serikali katika kuimarisha Sekta ya Elimu.









# NATAKA KUONA KILA KATA INAKUA NA KITUO CHA MAFUNZO KWA WALIMU – DKT.MSONDE

**Na Mwandishi Wetu – Morogoro.**



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Elimu, Dkt. Charles Enock Msonde, amesema anataka kuona kila Kata hapa nchini inakua na Kituo cha Mafunzo kwa Walimu ili kuwawezesha walimu hao kuendelea kujifunza wakati wote.

Dkt. Msonde aliyasema hayo wakati wa kufunga Mafunzo Rejea ya Usimamizi wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini kwa Viongozi na Waratibu wa Mpango wa MEWAKA ngazi za Mikoa na Halmashauri.

Alisema kuwa anataka kuona mafunzo kwa Walimu yanaendelea kila siku hivyo kutaka vituo hivi kuwepo katika kila Kata kwani itasaidia Walimu kuongeza ujuzi na kuwa mahiri katika jukumu lao kubwa na muhimu sana la kumuelimisha mtoto wa Kitanzania.

"Nataka kuona Walimu kwenye Kata wanabainisha changamoto zao za Kitaaluma na kupitia vituo vya MEWAKA changamoto hizo zinatatuliwa." Alisema Naibu Katibu Mkuu huyo anayeshughulikia Elimu.

Wakati huohuo, Dkt. Msonde aliwaelekeza viongozi wote waliohudhuria mafunzo hayo kwenda kusimamia utekelezaji wa mafunzo kuanzia ngazi ya mikoa hadi kwenye kata na wawe wanakutana kufanya marejeo ya vigezo vya utekelezaji wa Mpango wa MEWAKA.

Hali kadhalika aliwataka viongozi hao kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kutoka kwa Walimu ili kufahamu kwa kina kila ambacho kinahitajika katika kujenga uwezo wa Walimu na sio kukaa Ofisini na kuandika yale wanayoyajua wao.

Aidha, Dkt. Msonde aliagiza Mpango wa MEWAKA kwa kila Halmashauri uwe wazi na kila kiongozi ajue changamoto zinazowakabili Walimu wao na nini wanapashwa kufanya katika shule zao hii itasaidia katika utekelezaji wa Mpango wa MEWAKA.

Mwisho aliwataka viongozi hao kushirikiana katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango huo ili kuboresha elimu nchini.



# NATAKA KUONA KILA KATA INAKUA NA KITUO CHA MAFUNZO KWA WALIMU – DKT.MSONDE













# NATAKA KUONA KILA KATA INAKUA NA KITUO CHA MAFUNZO KWA WALIMU – DKT.MSONDE













# WALIMU WATAKIWA KUONGEZA KASI YA UFUNDISHAJI KUFUTA DARAJA SIFURI

**Na Mwandishi wetu – Singida.**



*Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba akizungumza katika kikao kazi kilichowakutanisha Walimu wa shule za msingi, sekondari na wadhibiti ubora kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa RC Mission uliopo mjini Singida hivi karibuni.*

Walimu wa shule za Serikali mkoani Singida wametakiwa kuhakikisha wanafuta daraja la sifuri na daraja la nne kwa kufanya kazi kwa bidii, kuwashirikisha wazazi na wanafunzi wenyewe.

Agizo hili limetolewa na Mkuu wa Mkoa (RC) wa Singida, Peter Serukamba katika kikao kazi kilichowakutanisha Walimu wa shule za msingi, sekondari na wadhibiti ubora kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa RC Mission uliopo mjini Singida hivi karibuni.

RC Serukamba amesema uondoaji wa madaraja hayo ya elimu utawezekana kwa kuacha uzembe, kuwahi kazini na kuwa na tabia ya kupata mrejesho baada ya kufundisha huku akiwataka wazazi kuhakikisha wanafunzi wanapata chakula shuleni.

Hata hivyo, amewataka Maafisa elimu wa kata kuhakikisha wanatembelea shule na kuhakikisha kila mwalimu anatimiza majukumu yake huku akiwakumbusha wadhibiti ubora kutowadhibiti walimu pekee badala yake waangalie changamoto zinazo wakabili walimu na kuzitafutia ufumbuzi.



*Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Mwl. Dorothy Mwaluko akisisitiza jambo wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha Walimu wa shule za msingi, sekondari na wadhibiti ubora kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa RC Mission uliopo mjini Singida hivi karibuni.*

Aidha amewakumbusha walimu kahakikisha kwamba katika Mkoa wa Singida hakutakuwa na mwanafunzi atakayemaliza darasa la Saba bila kujua kusoma na kuandika.

Katika kuboresha Elimu, RC Serukamba ameeleza nia yake ya kutaka kuanzisha mashindano kwa Shule za Sekondari ambapo shule ambayo haitapata daraja sifuri na daraja la nne watapata zawadi itakayo gawanywa kwa walimu wote wa shule husika.

"Umefika wakati sasa wadhibiti ubora kuhakikisha tunapata elimu bora kwa kuwa Serikali imeshawekeza vya kutosha katika

# WALIMU WATAKIWA KUONGEZA KASI YA UFUNDISHAJI KUFUTA DARAJA SIFURI

majengo na miundombinu ya shule, umefika wakati Serikali kuwekeza katika ujuzi ili kuleta ubobezi katika masomo yanayofundisha" alieleza RC Serukamba.

Hata hivyo amewataka walimu kuendeleza juhudi na utamaduni wa kusoma vitabu badala ya kutumia mitandao ya kijamii.

Kwa upande wake Katibu Tawala Mkoa wa Singida Mwl. Dorothy Mwaluko amesema Mkoa una jumla ya Walimu 7492 ambapo wa shule ya msingi ni 5166 na Sekondari ni Walimu 2326.

Amesema uwepo wa walimu hao umesababisha kuanza kuboresha elimu ambapo amesema kwa kidato cha sita ufaulu umefikia daraja la kwanza na kwa wanafunzi wa darasa la nne ameeleza kwamba waliofanya mtihani ni asilimia 93 na waliofaulu ni asilimia 82.

Hata hivyo Katibu Tawala huyo amesema katika zoezi la kuboresha elimu mkoani hapo tayari wameanzisha mkakati maalum ambapo utaboresha mahudhurio ya Walimu na Wanafunzi, ujenzi wa miundombinu na kuboresha uwajibikaji.

Aidha Mwaluko amesema tayari wameshaanza mafunzo ya Walimu ambapo jumla ya Walimu 1972 kati ya 7000 wameaanza kupata mafunzo ya kuwajengea uwezo.

Naye Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi TAMISEMI Suzan Nusu ameagiza kuendelea kutolewa kwa Mafunzo endelevu ya walimu kazini (Mewaka) ndani ya shule ili kujengeana uwezo na kuboresha Elimu na ufundishaji.

Mkutano huo ulihudhuriwa na jumla ya walimu 1956 kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Singida na kuhusisha walimu wa shule ya msingi, sekondari, Tume ya Utumishi wa walimu na wadhibiti ubora.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.



*Washiriki wa kikao kazi kilichowakutanisha Walimu wa shule za msingi, sekondari na wadhibiti ubora kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa RC Mission uliopo mjini Singida hivi karibuni wakiwa katika hali ya furaha wakati wa kikao kazi hicho.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Katibu Wasaidizi wa TSC wa Wilaya za Mkoa wa Singida.*

# TSC YASHAURIWA KUFANYA TAFITI KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



*Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulia Elimu katika Mkoa wa Morogoro, Mwl. Germana Mng'aho akitoa hotuba ya kufunga Kikao Kazi cha Wadau wa Elimu cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.*

**Na Mwandishi Wetu – Morogoro.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeshauriwa kufanya tafiti ndogondogo kubaini aina na sababu za makosa yanayotendwa na walimu kwa kuzingatia umri wao ili kuweza kusaidia walimu kujiepusha na vitendo vya ukiukaji wa maadili ya taaluma hiyo.

Ushauri huo umetolewa hivi karibuni na Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulia Elimu katika Mkoa wa Morogoro, Mwl. Germana Mng'aho wakati akifunga Kikao Kazi cha Wadau wa elimu kilichofanyika mjini Morogoro kwa lengo la kufanya mapitio ya Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu.

Alisema kuwa kuna uwezekano kuwa yapo makosa yanayofanywa na walimu kutokana na umri wao kwa kuwa wengi wanajiriwa wakiwa na umari mdogo, hivyo tafiti zikifanyika zitasaidia kuweka mikakati ya kuzuia kutendeka kwa makosa hayo ambayo yanasababisha walimu kuchukuliwa hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa kazi.

"Kuna haja kwa Tume kufanya tafiti ndogondogo kugundua makosa yanasababishwa na nini ili tuweze kuyazuia. Unajua wakati mwingine makosa haya yanaendana na umri tu, walimu wengi wanaajiriwa wakiwa na umri mdogo na kama tunavyojua kwenye umri wa ujana kuna changamoto zake. Tunahitaji



*Mwenkiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulia Elimu katika Mkoa wa Morogoro, Mwl. Germana Mng'aho ili afunge Kikao Kazi cha Wadau wa Elimu cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.*



*Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Fatuma Muya akitoa neno la utangulizi wakati wa kufunga Kikao Kazi cha Wadau wa Elimu cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni.*

# TSC YASHAURIWA KUFANYA TAFITI KUZUIA UKIUKWAJI WA MAADILI KATIKA UTUMISHI WA WALIMU



*Wadau wa Elimu walioshiriki Kikao Kazi cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni wakiwa ukumbini wakati wa kufunga kikao kazi hicho.*

kuyajua yote hayo ili tuzuie walimu wetu kuingia kwenye makosa. Nia yetu ni kujenga walimu bora ili nao waweze kutengeneza wanafunzi bora katika katika taaluma na maadili," alisema Germana.

Alieleza kuwa kuna matukio yanayofanywa na waalimu wachache ambayo yanatia dosari heshima na hadhi ya taaluma ya ualimu huku akieleza kuwa suala mahusiano ya kimapenzi kati ya mwalimu na mwanafunzi ni jambo linalotakiwa kukemewa kwa nguvu zaidi kwa kuwa vitendo hivyo bado vinaendelea kutokea.

Alifafanua kuwa wazazi, jamii na Serikali kwa ujumla inaamini kwamba mtoto anapokuwa mikononi mwa mwalimu yupo salama, hivyo TSC ina wajibu kuhakikisha mwalimu akikabidhiwa mtoto jukumu lake ni kumlea katika nyanja zote na kamwe asiwaze kumfanya kuwa mpenzi wake.

Alisema kwa kuwa TSC imepewa jukumu la kusimamia maadili ya walimu kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, Serikali inatarajia kuona kazi kubwa ikifanyika katika kuzuia utovu wa nidhamu kwa kutoa elimu juu ya masuala yote yanayohusu utumishi wa Walimu na Utumishi wa Umma.

Aliendelea kueleza kuwa, Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu ambapo kazi hiyo imefadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa BOOST utasaidia walimu kuelewa kanuni hizo kwa urahisi zaidi, hivyo TSC ihakikishe kuwa walimu wote wanapatiwa elimu juu ya ufafanuzi huo.

"Napenda kuipongeza Tume kwa namna ilivyojipanga kutekeleza mradi wa BOOST, ninaamini mtaleta mapinduzi makubwa kwenye elimu hususan katika kuimarisha maadili na nidhamu ya walimu wetu. Lazima tuhakikishe walimu wetu wanakuwa na uelewa wa kutosha juu ya ufafanuzi huu ili watekeleze majukumu yao kama inavyotakiwa ili tuwe na shule salama," alisema.



*Wadau wa Elimu walioshiriki Kikao Kazi cha kupitia Rasimu ya Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu kilichofanyika mjini Morogoro hivi karibuni wakiwa ukumbini wakati wa kufunga kikao kazi hicho.*



**MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA**
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz** **Tovuti: www.tsc.go.tz**

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania tumeyautumishiwawalimutanzania